# HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA

## KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA KUPITIA TAARIFA YA MWEZI OKTOBA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

## KIKAO KITAKACHOFANYIKA TAREHE 17/11/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI (PAULINE).

***Imetayarishwa Na:***
***Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,***
***S.L.P 22,***
***MAHENGE/ULANGA.***
**BARUA PEPE: ded@ulangadc.go.tz**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA KUPITIA TAARIFA YA ROBO YA KWANZA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KILIFANYIKA TAREHE 25/10/2021**

## 1. MAHUDHURIO

### 1.1 Wajumbe Waliohudhuria

| C/N | JINA | IDARA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Edson Solly | Diwani Kata ya Mwaya | Mwenyekiti. |
| 2. | Ndg.Saida Mahugu | Mkurugenzi | Katibu |
| 3. | Mh. Salim A.Hasham | Mbunge Jimbo la Ulanga | Mjumbe |
| 4 | Mh. Yahaya Fundi | Diwani Kata ya Chirombola | Mjumbe |
| 5. | Mh. Novatus Majiji | Diwani kata ya Lukande | Mjumbe |
| 6. | Mh.Deogratias Akilimali | Diwani kata ya Uponera | Mjumbe |
| 7. | Mh. Amina Seif Mgelwa | Diwani kata ya Lupiro | Mjumbe |
| 8. | Mh. Emanuel Langisi | Diwani kata ya iragua | Mjumbe |
| 9. | Mh. Venance S. Chatu | Diwani kata ya Isongo | Mjumbe |
| 10. | Mh. Hawa Mgaichuma | Diwani Viti Maalumu Lupiro | Mjumbe |
| 11. | Mh. Tarsis Noya | Diwani kata ya Sali | Mjumbe |

### 1.2 Wajumbe Waliohudhuria

| C/N | JINA | IDARA | CHEO |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndg. Veronica Marwa | DHRO | Mtaalamu |
| 2. | Ndg. Juma Kapilima | DLFO | Mtaalamu |
| 3. | Ndg. Burton Mahenge | Ag.DAICO | Mtaalamu |
| 4. | Ndg. Devotha Kisembo | Ag.DLO | Mtaalamu |
| 5. | Ndg. Jasmine Mlyandi | Ag. DTO | Mtaalamu |
| 6. | Ndg.Zawadi Mtatifikolo | Ag.DLUPO | Mtaalamu |
| 7. | Ndg. Ntigonza Jonas | Ag. DSEO | Mtaalamu |
| 8. | Ndg. Yuster Sengo | Ag. IO | Mtaalamu |
| 9. | Ndg. Lucy Ngailo | Ag.DPEO | Mtaalamu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. | Ndg. Mohamed Atiki | DCDO | Mtaalamu |
| 11. | Ndg. Ambroce Majumba | DT | Mtaalamu |
| 12. | QS. Amiry Muchumbuye | DE | Mtaalamu |
| 13. | Dr. Ally Mjema | DMO | Mtaalamu |
| 14. | Ndg. Sawia Ntiburela | AG. DBO | Mtaalamu |
| 15. | Ndg. Gilbert Martine | HPMU | Mtaalamu |
| 16. | Ndg. Justin Bundu | DESO | Mtaalamu |
| 17. | Ndg. Methew Festo | Ag. DICTO | Mtaalamu |
| 18. | Ndg. Florencia Michael | DNRO | Mtaalamu |
| 19. | Ndg.Bakari Liguguda | Ag. DIA | Mtaalamu |
| 20. | Ndg.Engilbert Kanyakanya | PSSNC | Mtaalamu |
| 21. | Damas Debwa | DPLO | Mtaalamu |

### 1.3. MWANDISHI WA KIKAO

Anastazia Mchukwa

### KUMB.NA. 01/10/2020 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 04:08 Asubuhi kwa kuwataka wajumbe kujadili hoja kwa kina na kufikia muafaka unaolenga maslahi mapana ya Halmashauri na wananchi kwa ujumla.

### KUMB.NA.02/10/2020 KUTHIBITISHA AGENDA

**Wajumbe waliridhia Agenda zifuatazo zijadiliwe kwenye kikao hicho**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha tarehe 15/09/2021
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha tarehe 15/09/2021
5. Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Mwezi Septemba 2021/2022
6. Kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji Kiidara Robo ya kwanza 2021/2022.
7. Kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya kwanza 2021/2022.
8. Kupokea na kujadili utaratibu wa kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga Msimu wa Kilimo 2021/2022.

iii. Mbegu zote zitakuwa katika kituo kimoja cha kuuzia ambapo mapendekezo ni katika ofisi ya Kilimo (W)

iv. Mbegu zitauzwa kwa wakulima wa wilaya ya Ulanga tu na si vinginevyo hivyobasi kutakuwa na rejista ya wakulima wote watakao nunua mbegu ambayo itaonesha na mahali ambapo shamba lipo ili kurahisha ufuatiliaji kwa ujumla wake.

Wajumbe walipokea mapendekezo hayo na kuyapitisha huku wakihimiza ununuzi wa pembejeo hizo kufanyika kwa wakati, mbegu zifike kwa msimu husika, ifikapo tarehe 30/11/2021 mbegu ziwe zimenunuliwa.

**KUMB.NA.09/10/2021 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA YA TSH 1,445,617,139.58 NJE YA BAJETI KATIKA ROBO YA KWANZA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

Mkuu wa Idara ya Mipango aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ilipokea jumla ya fedha **Tshs. 1,445,617,139.58** nje ya bajeti yake. Katika fedha hizo **Tshs. 1,410,000,000/=** ni kutoka "Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO -19 (IMF)" – ikiwa ni fedha za mkakati wa IMF kuchangia kufufua uchumi kwa sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya Elimu. Mgao ni kuwa – Elimu Msingi vituo shikizi – **Tshs 480,000,000.00** na Elimu Sekondari **Tshs. 840,000,000.00.** Sambamba na fedha hizo, pia halmashauri ilipokea **Tshs. 90,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1 ya waganga (3 in 1). Aidha zilipokelewa **Tshs 35,617,139.58** kwa ajili ya kujenga "miundombinu ya uvunaji maji mvua" katika shule 2 za Msingi na 1 ya sekondari.

**1. MCHANGANUO WA FEDHA – Tshs - 1,445,617,139.58.**

**(i) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 24 katika vituo shikizi sita tshs. 480,000,000.00**

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ina Vituo Shikizi **10**. Kati ya hivyo kuna Vituo Shikizi **3** vipo katika Bonde Oevu, havifai kwa matumizi ya kibinadamu ambavyo ni **Mbenja, Kipingu** na **Itobanilo**. Aidha Kituo kimoja cha **Kitonga** chenye watoto **40** kipo maeneo ya milimani, ambapo ni maeneo hatarishi, na vituo sita (**6**) vipo katika maeneo yanayoweza kuendelezwa kwa utoaji wa huduma za kijamii.

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ilipokea fedha kiasi cha Tshs. **480,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **24** kwenye Vituo Shikizi **4** ambavyo ni Mbenja madarasa **7** Tshs. **140,000,000/=** , Kanyaga-twende madarasa **7** Tshs.**140,000,000/=,**Itobanilo madarasa **4** Tshs. **80,000,000/=,** Kisaki Mbali madarasa **6** Tshs. **120,000,000/=**

**Mgawo kama ulivyotoka TAMISEMI**

| SHULE - SHIKIZI | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MKOA | HALMASHAURI | KITUO SHIKIZI | KITUO MAMA | IDADI | FEDHA | Payment Description |
| MOROGORO | Ulanga DC | Mbenja | Namhanga | 7 | 140,000,000.00 | Ujenzi Madarasa |
| | Ulanga DC | Kanyaga twende | Minepa | 7 | 140,000,000.00 | Ujenzi Madarasa |
| | Ulanga DC | Itobanilo | Minepa | 4 | 80,000,000.00 | Ujenzi Madarasa |
| | Ulanga DC | Kisaki mbali | Mbuyuni | 6 | 120,000,000.00 | Ujenzi Madarasa |
| | JUMLA | | | | 480,000,000.00 | |

Kutokana na Vituo viwili vya **Mbenja na Itobanilo kuwepo kwenye bonde oevu** fedha yake inatakiwa ihamishwe kwani eneo hilo halifai kwa shughuli za kibinadamu. Hivyo iombwe idhini ya kuhamisha fedha katika vituo hivyo na kufanya mabadiliko ya kupeleka fedha katika Vituo Shikizi vyote sita **(6)** badala ya Vituo nne (**4** ) vilivyopendekezwa ili kila kituo kinachostahili kuendelezwa kipelekewe madarasa manne kwa kila kituo ili viweze kusajiliwa vituo 6 kwa lengo la kupunguza umbali kwa wanafunzi.

**Jedwali la mchanganuo.**

| MAPENDEKEZO YA HALMASHAURI - MGAWO MPYA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S/N | KATA | SHULE MAMA | KITUO SHIKIZI | IDADI YA WANAFUNZI | VYUMBA | KIASI FEDHA | HALI HALISI YA KITUO |
| 1 | IRAGUA | IRAGUA KATI | MIKOCHI | 928 | 4 | 80,000,000.00 | MADARASA 4 YAMEKAMILIKA NA MADARASA 2 YAPO KWENYE HATUA YA BOMA . |
| 2 | MILOLA | MAVIMBA | TULIZA MOYO | 153 | 4 | 80,000,000.00 | VIBANDA 2 VYA NYASI. |
| 3 | MILOLA | MAVIMBA | IGAMBA | 147 | 4 | 80,000,000.00 | VIBANDA 2 VYA NYASI. |
| 4 | MINEPA | MINEPA | KANYAGATWENDE | 416 | 4 | 80,000,000.00 | WANAEZEKA MADARASA 2 |
| 5 | MINEPA | MBUYUNI | KISAKI MBALI | 225 | 4 | 80,000,000.00 | WAMESAFISHA NA KUANZA KUSOGEZA MATOFALI NA WANA VYUMBA 5 VYA NYASI. |
| 6 | LUKANDE | LUKANDE | MWANZI | 94 | 4 | 80,000,000.00 | WANA VYUMBA 4 VYA NYASI NA WAMEANZA KUFYATUA TOFALI. |
| JUMLA KUU | | | | 1963 | 24 | 480,000,000.00 | |

**(ii) Ujenzi wa madarasa ya kupokea kidato cha kwanza Januari 2022 Tshs. 840,000,000.00**

Mkuu wa Idara ya Mipango aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ilipokea orodha ya shule za Sekondari zitazonufaika na mgao wa ujenzi wa vyumba 42 vya madarasa kwa

ajili ya kupokea Kidato cha Kwanza 2022. Madarasa hayo yanatakiwa kuwa na jumla ya thamani ya **Tsh 840,000,000.00**.

**(iii) FEDHA TSHS. 90,000,000.00 ZA COVID -19 (IMF) – UJENZI WA NYUMBA YA 1 WAGANGA (3 in 1).**

Sambamba na fedha za kujenga miundombinu ya sekta ya Elimu, pia Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs. 90,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya waganga 1 – (3 in 1). Maelekezo yaliyotoka katika kikao kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa kilichofanyika tarehe 17/10/2021, yalielekeza nyumba hivyo kujengwa katika Hospitali za Wilaya.

**FEDHA ZA RWSSP ZA KUJENGA MIUNDOMBINU YA UVUNAJI MAJI YA MVUA TSHS. 35,617,139.58**

Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ilipokea mgao wa fedha wa **Tshs. 35,617,139.58** za kujengea **miundombinu ya "uvunaji wa maji ya mvua"** katika shule tatu kwa mchanganuo ufuatao;
Aidha,kutokana na fedha hizo kupokelewa nje ya bajeti, aliiomba Menejimenti kutoa idhini ya kuomba vifungu kwa ajili ya matumizi ya fedha hizo.

Wajumbe waliipitisha taarifa hiyo kwa makubaliano kwamba madarasa mawili ya fedha za mapato ya ndani yatoke Lupiro Sekondari na kuelekezwa Igota Sekondari, Halmashauri ya kijiji itajenga vyoo matundu manne ili sekondari hiyo kuweza kufanya kazi, aidha katika suala la shule shikizi wajumbe walikubaliana na maoni ya Menejimenti na kutaka mchakato wa kuomba vifungu na idhini ya kuhamisha vituo kuendelea.

**KUMB.NA.10/10/2021 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA MAPENDEKEZO YA VYANZO VIPYA VYA MAPATO VITAKAVYOSIMAMIWA NA IDARA YA AFYA.**

Afisa Afya Mazingira aliwasilisha hoja kuwa kufuatia maelekezo ya Serikali ya kutaka kila Halmashauri kusimamia kikamilfu suala la ukusanyaji wa mapato kila idara/kitengo ilitakiwa kuwasilisha/kuibua vyanzo vipya vya mapato vitakavyoiwezesha Halmashauri kukusanya maduhuli yake kwa ajili ya kujiendesha.
Kwa mujibu wa sheria namba 1 ya Afya ya Umma ya mwaka 2009 kifungu cha saba (7) kinaeleza majukumu ya Afisa Muidhiniwa pia kifungu namba sita (6) kinaipa mamlaka Halmashauri ya kutunga sheria ndogo ili kuwezesha utekelezaji wa huduma za Afya inayohusiana na mambo yote yanayohusu Afya ya Umma.
Miongoni mwa majukumu ya Afisa Muidhiniwa yaliyoainishwa kwenye kifungu cha Saba (7) ni kufanya ukaguzi kwenye maeneo mbalimbali na kutoa ushauri wa kitaalam (Consultation). Hivyo basi, kama ilivyo kwenye maeneo mengine ushauri huo hutolewa kwa malipo. Hivyo aliwasilisha taarifa ya mapendekezo hayo kwenye kamati ya usimamizi wa Halmashauri CMT ili yaweze kupitiwa na kutolewa maamuzi.
Baada ya wajumbe kupitia mapendekezo hayo waliomba wapate muda kwa ajili ya kupitia taarifa hiyo na kisha kujadiliwa katika kikao kijacho.

**KUMB. NA. 14/10/2021 KUFUNGA KIKAO**
Kikao kilifungwa mnamo saa 10:32 Jioni baada ya kuhimiza Menejimenti kujitahidi kufuta na kupunguza hoja za Ukaguzi wa Ndani.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA**

| | |
|---|---|
| **JINA: SAIDA MAHUGU** | **JINA: EDSON W. SOLLY .** |
| SAINI: ............................ | SAINI: ................................ |
| **KATIBU.** | **MWENYEKITI.** |
| TAREHE: 17/11/2021 | TAREHE: 17/11/2021 |